
# English - Swahili Dictionary of Meteorological Terms

# Kamusi ya Kiingereza - Kiswahili ya Istilahi za Hali ya Hewa



## Kenya Meteorological Department

## FORWARD AND ACKNOWLEDGEMENT

Kenya Meteorological Department (KMD) and the Adaptation Consortium conducted a survey to examine the slow mainstreaming of climate information services (CIS) by the intended users, in planning and decision-making. This was despite the fact that KMD has religiously provided information hourly for some sectors, daily, weekly, monthly and seasonally. The results revealed that lack of understanding of the CIS content, accessibility and channels of communication as a reason for the low uptake of information. This was mainly because in most cases the language used is English, selection of dissemination channels were not appropriate for some communities and therefore inhibiting access.

It is in this respect that KMD with support from Adaptation Consortium through DFID funding engaged a consultant to translate some common meteorological terms used in disseminating CIS from English to Kiswahili, (a national language) in an effort to improve understanding the CIS content. This is after successfully translating of the same terms in Kikamba language used in Makueni, Machakos and Kitui.

The consultant's report or translation (Kamusi= Kiswahili dictionary)  could not be used straight away without involving the stakeholders as it is a requirement in the constitution that before any document or policy is used for consumption by the public, stakeholders must be consulted and their opinion sought. The stakeholders include the general public, extension agents, farmers, media and climate scientists.

Stakeholders held a one-day workshop and deliberated on the translation (Kamusi). The aim of the workshop was to ensure the language used is the common Kiswahili spoken by the common person likely to receive and use the climate information.

It is hoped that this exercise will continue until we have a dictionary for all or a least major community languages in the country and, improve the understanding of CIS and increase uptake, especially at the local level.

On behalf of the Kenya Meteorological Department, I wish to thank the following organisations and groups for allowing their officers to participate

in this noble exercise of validating the translation of meteorological terms to Kiswahili; Royal Media Service, Nation Media Group, Kenya Broadcasting Corporation, The Kenya Agricultural and Livestock Research Organization researchers, The Undugu Kenya Communications Officer, Machakos Farmer's representative, Gallababu Consultant Ltd, KMS staff and NDMA staff.

KMS is committed to work with stakeholders to improve climate information service delivery to all communities in the country.

KMD wishes to acknowledge the translators and reviewers of the Kamusi listed below for their valuable time to make this very important document available to stakeholders.

**Translators**

1. Hamisi O. Babusa
2. Martha M. Mutua
3. Ali Hassan Kauleni

**Reviewers**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mr. Jack Silvester Oloo | Swahili Broadcaster - KBC Nairobi |
| 2. | Dr. Ken Walibora | Swahili Broadcaster - QTV Nairobi |
| 3. | Ms. Mwanahamisi Hamadi | Swahili Broadcaster - CTV Nairobi |
| 4. | Peter O. Abiya | Communications Officer NDMA, Nairobi |
| 5. | Priscilla Arungo | County Director of Agriculture, Machakos |
| 6. | Mr. Samuel Mwangi | Climate Scientist KMD, Nairobi |
| 7. | Mr. Ayub Shaka | Climate Scientist KMD, Nairobi |
| 8. | Dr. Richard Muita | Climate Scientist KMD, Nairobi |
| 9. | Mbai Mukuyu | Farmers in Machakos |
| 10. | N.Emerita | Researcher KARLO, Katumaini - Machakos |
| 11. | Consolata Asin | Communications Officer, Undugu Society Nairobi |

James G. Kongoti

Director of Meteorological Services and Permanent Representative of Kenya with the World Meteorological Organization (WMO)

# A

**Above average** Kiwango kinachozidi wastani.

**Above normal** Kiwango kinachozidi kawaida.

**Acid rain** Mvua;asidi: mvua ambayo huwa imechanganyika na kemikali zenye asidi zilizoko kwenye anga hewa na kufanya maji yake kudhuru mimea na viumbe wa tumiao maji hayo.

**Advection** Hali ya kusafirishwa kwa kitu chochote kile kilichoko kwenye anga hewa na upepo.

**Advisory** Ushauri wa kitaalam kuhusu jambo fulani; kwa mfano hali ya hewa.

**Air** Hewa.

**Air; mass** Masi;hewa: ni mkusanyiko wa hewa wenye unyevun yevu na halijoto fulani unaopatikana katika sehemu fulani.

**Air pollution** Mchafuko wa hewa.

**Air pressure** Kanihewa: shinikizo la uzito wa hewa kwenye ardhi. Shinikizo hili huwa tofauti katika maeneo mbalimbali.

**Altitude** Mwinuko: kipimo cha eneo fulani kulingana na kuinu - ka kwake kutoka kwa kima cha bahari.

**Anabatic wind** Upepo;mpanda: ambao huvuma kutoka kwenye bonde hadi juu mlimani baada ya hali joto yake kupanda juu na kusukumwa na upepo baridi ulio chini ya mlima.

**Anenometer** Kipima;upepo: kifaa kinachotumiwa na wanasayansi kupimia kasi ya upepo.

**Anticyclone** Kitenguakimbunga: sehemu ambayo huwa na shini -

kizo;hewa la hali ya juu na aghalabu hali ya hewa yake huwa tulivu.

**Anvil** Wingu;fuawe: sehemu ya juu ya mawingu aina ya kumulonimbasi ambayo huwa bapa na hufanana na fuawe. [taz. cumulonimbus]

**Anvil crawler** Mtambaa;fuawe: aina fulani ya mfyatuko wa umeme ambao huonekana kutambaa kutoka kwenye wingu;fuawe kunaponyesha mvua ya radi.

**Atmosphere** Anga;hewa: sehemu ya juu ya sayari ambayo imezungukwa na hewa; kwa mfano anga;hewa ya dunia imegawanyika katika sehemu tano.

# B

**Backing winds** Pepo;boko: aina za pepo ambazo hubadili welekeo wake na kwenda kinyume na welekeo wa saa katika eneo.

**Barometer** Kipima;kanihewa: kifaa kinachotumiwa na wanasayansi kupimia kanihewa.

**Barometric pressure** Kanihewa: shinikizo la uzito wa hewa kwenye ardhi. Shinikizo hili huwa tofauti katika maeneo mbalimbali.

**Below average** Chini ya kiwango cha wastani.

**Below normal** Chini ya kiwango cha kawaida.

**Bow echo** Mwangwi;pinde: mwangwi wa rada wenye umbo la mstari ambao umepinda kama uta na aghalabu huhusiana na hali mbaya ya hewa.

# C

**Calm** Shwari/tulivu: kipindi ambapo hali ya hewa huwa tulivu yaani pasipo upepo au mvua.

**Cirrus clouds** Mavundemavunde: aina ya mawingu mepesimepesi yenye umbo la nyuzinyuzi ambayo huwa juu sana angani.

**Clear** Anga kavu: hali ambapo anga huonekana tupu kwa kukosa mawingu. Kwa mfano, katika kipindi cha ukame.

**Climate change** Mabadiliko ya wastani wa hali ya hewa: mabadiliko ya ruwaza za hali ya hewa kama vile; mvua, halijoto, kutanda kwa mawingu n.k. katika eneo fulani kwa muda wa miaka thelathini ama zaidi.

**Climate information service (CIS)** Huduma ya Habari za Hali ya Hewa.

**Climate outlook** Hali ya kijumla ya utabiri wa hali ya hewa katika msimu fulani.

**Climate variability** Kubadilikabadilika kwa hali ya hewa katika misimu mbalimbali.

**Climate** Wastani wa hali ya hewa: wastani wa jumla wa hali ya hewa katika eneo fulani, katika majira fulani.

**Cloud bank** Mawingu yaonekanayo kwa mbali.

**Cloud burst** Mvua kubwa inayonyesha kwa muda mfupi na aghalabu huandamana na dhoruba na mawe.

**Cloud streets** Safu za mawingu: safu ambazo huwa katikati ya

mawingu aina ya mavundemavunde aghalabu huonekana vizuri zaidi kwenye picha za setilaiti kuliko jinsi zitakavyoonekana kwa kuzitazama tu kutoka ardhini.

**Cloud** Wingu: Mvuke ambao umepaa angani na kuchukua umbo fulani.

**Coastal flooding** Mafuriko ya pwani.

**Comma echo** Mwangwi; koma: mwangwi wa rada unaoshuhudiwa wakati wa mvua ya radi na aghalabu una mkao wa alama ya koma.

**Common Alert Protocol** Itifaki ya usambazaji wa ilani: utaratibu wa usambazaji wa ilani ya hali ya hewa.

**Composite** Mchanganyiko.

**Convection** Myuko: Hali ya kukipa kimiminika joto jingi hadi kipae angani.

**Crystalization** Gandisha: hali ya molekyuli kuungana na kuwa ngu-mu na hali ya chembechembe kama za chumvi.

**Cumulonimbus clouds** Mawingu chamchela, Kumulonimbasi: mawingu mazito ambayo huwa yamesimama wima na aghalabu husababisha mvua kubwa ya radi.

**Cumulus clouds** Mawingu;pamba: mawingu yenye umbo la pamba yaliyopangika kwenye anga na aghalabu huwa ni -ishara ya halitulivu ya hewa.

**Cyclone / hurricane/ typhoon Tufani/ kimbunga:** jina la kijumla lina lorejelea upepo mkali ambao huleta madhara makubwa.

# D

**Debris** Vifusi: mtapanyiko wa mabaki ya vitu vilivyosombwa na nguvu za upepo au maji na kuvunjwavunjwa na kuharib-iwa kabisa.

**Dense fog** Ukungu mzito: hali ya hewa kuwa na uvundevunde au unyevu.

**Dew point** Kiwangoumande: Kiwango cha hali;joto ambapo hewa hugeuka na kuwa umande.

**Dew** Umande; matone madogomadogo ya maji ambayo huanguka juu ya ardhi na nyusoni mwa vitu vinginevyo kama vile nyasi, majani ya miti ambavyo huwa nje hasa wakati wa usiku.

**Divergence** Mtawanyiko;panda: hali ya masi;hewa kutawanyika kwa umbo la njia panda.

**Downscaling** Uzingatiaji wa kina wa hali ya hewa ya sehemu mahususi

**Downslope wind** Upepo wa uwandani: upepo unaofululiza kutoka seh emu ya juu na kushuka uwandani.

**Drizzle** Manyunyu: aina ya mvua ambayo huwa ni nyepesi sana na aghalabu hunyesha kwa matone madogomadogo na mtu anaweza kutembea ndani ya mvua bila kulowa.

**Drought resistance** Uwezo wa kustahimili ukame.

**Drought** Ukame/ukavu: hali ambayo mvua hupungua kwa muda mrefu hivyo kuifanya ardhi ikauke. Hali hii husababisha upungufu wa maji na chakula.

**Dust/ sandstorm** Vumbi/dhoruba ya vumbi: upepo unaovuma kwa ngu vu na kusababisha vumbi hasa jangwani na kuathiri uwezo wa kuona mbali.

# E

**Eclipse** Kupatwa kwa mwezi au jua: solar eclipse; kupat wa kwa jua; hali ya dunia, mwezi na jua kuwa katika msitari mmoja na hivyo mwezi kuziba mwangaza wa jua usifike duniani, lunar eclipse; kupatwa kwa mwezi; ni hali ya kivuli cha dunia kutoka mwangaza wa jua kunguka juu ya mwezi na kuzima mwangaza wake kwa muda fulani.

**El Niño** Elininyo: hali ya kupanda kwa halijoto katika Bahari ya Pasifiki kuliko kiwango cha kawaida inayosababi-sha mabadiliko ya mikondo ya kawaida ya pepo na aghalabu kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa.

**Equinox** Siku mlingano/ Ikwinokisi; wakati ambapo saa za mchana na za usiku hulingana na aghalabu jua huwa limevuka mstari wa Istiwahi; hali hii hutokea mara mbili katika mwaka : tarehe 21 Machi na tarehe 23 Septemba.

**Evaporation** Mvukizo: hali ya maji kubadilika na kuwa mvuke ku-tokana na kuzidishwa kwa halijoto.

**Evapotranspiration** Myuko;mvukizo: hali ya mvuke unaotoka kwenye majani ya miti, ardhini na maji ya bahari, maziwa na mito na kwenda kwenye angahewa.

# F

**Flash flood warning** Tahadhari kuhusu mafuriko ya ghafla.

**Flash floods** Mafuriko ya ghafla.

**Flood crescent** Kilele cha mafuriko.

**Flood forecast** Utabiri wa mafuriko: maelezo yanayotahadharisha watu kuhusu mafuriko

**Flood plain** Uwanda mai: sehemu ya ardhi ambayo huwa karibu na mto ambayo aghalabu hufurika msimu wa mvua.

**Flood** Furika: tendo la maji kujaa na kuvuka kingo za mto kutokana na mvua kubwa na kusababisha mafuriko.

**Floods** Mafuriko: hali ambapo maji huvuka kingo za mito kutokana na mvua kubwa.

**Fog** Ukungu mzito: aina ya mawingu mazito meupe ambayo hutanda ardhini na kusababisha hali ya gizagiza kama inavyokuwa asubuhi sana kabla ya mapambazuko. Hali hii huwafanya watu kutoona vizuri.

**Freezing rain** Mvua baridi: mvua ambayo matone yake ya maji yana baridi nyingi sana kama barafu.

**Front** Mpaka wa masi hewa: eneo ambapo aina mbili za masi hewa ambazo zina hali joto na uzito tofauti hukutana na kutengeneza kitu kama ukanda wa mawingu meupe hasa ikionekana katika picha ya setilaiti. Warm front: Ukanda wa masihewa vuguvugu. Pahali ambapo masihewa joto husukuma masihewa baridi. **Cold front**: Ukanda wa masihe wa baridi. Pahali ambapo masihewa baridi husukuma masihewa yenye vuguvugu.

**Frost** Sakitu: baridi kali inayosababisha theluji.

**Frostbite** Ukongo;jalidi: Ni kuathirika kwa ngozi au tishu za mwili zilizoko mbali na moyo kwa sababu ya kufa ganzi kutokana na baridi kali ya kipupwe.

# G

**Glaciation** Mto barafu: kutanda kwa barafu na kuenea mahali fulani kwenye nchi kavu.

**Glacier** Bonge la barafu; barafu ambayo huwa imeshikamana yenye umbo la duara na aghalabu hutengeneza donge kubwa, zito ambalo husonga pole pole kuelekea bondeni. haliyeyuki kwa urahisi hata kwa joto kali.

**Green house effect** Athari mvugulio. hali ambayo miale ya jua huingia pahali na kugeuka na kuwa vuguvugu ambalo hufungiwa na haliwezi kupita na kupanda juu.

**Greenhouse gasses** Gesi mvugulio. Aina za gesi kama vile,kaboni dayoksaidi na metheni ambazo hujenga utandu ambao hufungia joto lisipite na kupanda juu an gani.

# H

**Hail** Mvua ya mawe inayotokana na mawingu ya kumulo nimbasi.

**Hailstorm** Dhoruba ya ngurumo na radi inayosababisha mvua ya mawe.

**Heat wave** Wimbi la joto;vipindi virefu vya joto visivyo vya kawaida na aghalabu wakati mwingine huweza kuandamana na unyevu na hutokea kila mwaka na hudhuru watu.

**Heavy rain** Mvua kubwa; mvua inayonyesha kwa wingi.

**High pressure system** Mfumo wa juu wa kanieneo; bonge la hewa kavu; baridi ambayo huzunguka kwa kasi sana huku ikisababisha hali nzuri ya anga na aghalabu hushuhudiwa kule Kaskazini mwa Istiwahi ambapo ikitazamwa kutoka juu, upepo huwa unazunguka kutoka kwa kitovu sawia na saa.

**High probability** Uwezekano mkubwa wa kutendeka kwa jambo au kitu. kwa mfano, kuna uwezekano mkubwa wa kunye sha kwa mvua.

**High tide** Bamvua; hali ya kujaa kwa maji ya bahari.

**High wind** Upepo mkali; hewa ambayo huenda kwa kasi kuliko kawaida aghalabu hutoa mvumo katokana na kasi yake.

**High yield** Mavuno/Mapato mengi.

**Humidity** Unyevu; kipimo cha umajimaji ulioko katika hewa.

**Hydrology** Haidrolojia; sayansi inayochunguza masuala ya maji

**Hygrometer** Kipima unyevu; kifaa maalum kinachotumiwa kupimia umajimaji ulioko kwenye angahewa.

# I

**Ice** Barafu.

**Insolation** Mnunurisho wa sola; ile hali ya miali ya jua kuingia pahali.

**Inversion** Mgeuko; sehemu ya anga hewa ambapo halijoto huongezeka kadri kimo cha eneo hilo kinavyoongezeka

**Isobar** Isobaa; mstarikani ambao huchorwa katika ramani ili kuunganisha sehemu ambazo zina msukumo wa hewa ulio sawa.

**Isohyte** Mstari mvua; mstari unaochorwa kwenye ramani ya nchi au dunia kuashiria sehemu ambazo zina kiwango cha mvua sawa.

**Isotach** Mstari upepo ; mstari unaochorwa kwenye ramani ya nchi au dunia kuunganisha mahali kwenye kasi sawa ya upepo.

**Isotherm** Mstari halijoto; mstari ambao huchorwa katika ramani kuunganisha mahali kwenye kadri sawa ya halijoto.

## J

**Jet stream** Upepo Jeti; ukanda wa upepo mkali sana na aghalabu huvuma kwa kasi sana angani.

# K

**Katabatic wind** Upepo;mshuka: upepo ambao hubeba hewa yenye uzito kutoka juu mlimani na kuvuma kushuka bon-deni mara nyengine kwa kasi kwa sababu ya kuvut wa na nguvu za mwangusho.

# L

**La Niña** Laninya; hali ya kupungua kwa halijoto katika Bahari ya Pasifiki kuliko kiwango cha kawaida inayosababisha mabadiliko ya mikondo ya kawaida ya pepo

**Land breeze** Mwanashanga; upepo ambao huvuma kutoka nchi kavu kuelekea baharini au eneo jingine la maji kama vile ziwa hasa wakati wa usiku.

**Latent heat** Joto fiche; joto ambalo huhifadhiwa au kutolewa na vitu aina ya majimaji, mango au gesi wakati vinapobadilika kutoka hali yake halisi hadi hali nyingine hasa kutokana na kuongezeka au kupungua kwa hali joto; kwa mfano, maji yanapobadilika na kuwa gesi.

**Latitude** Latityudo/ latityudi; mstari wa kidhahania ambao huchorwa katika ramani kutoka mashariki kwenda magharibi na aghalabu huweza kutumiwa kupima umbali kutoka kaskazini au kusini mwa istiwahi.

**Leeward side** Demani; sehemu ambayo imekingwa na mlima kutokana na upepo unaovuma kutoka upande wa pili wa mlima na aghalabu hupata mvua chache M.f. mji wa Nanyuki uko demani mwa Mlima Kenya

**Light rain** Mvua nyepesi.

**Lightning** Radi; spaki au cheche kubwa sana za umeme ambazo hutoka mawinguni hadi ardhini hasa wakati wa mvua ya radi.

**Longitude** Longityudo/ longityudi: msitari wa kidhahania unaochorwa katika ramani kutoka kaskazini kwenda kusini na aghalabu hutumiwa kupima majira na umbali kutoka mashariki au magharibi.

**Low Pressure system** Mfumo wa chini wa kanieneo; bonge la hewa vuguvugu, lenye unyevunyevu ambalo aghalabu husababisha mvua iliyoandamana na dhoruba.

**Low probability** Uwezekano mdogo wa kutendeka kwa jambo

**Low tide** Maji mafu/ maji kupwa.

# M

**Mainly cloudy** Kipindi cha mawingu mengi.

**Mainly sunny** Kipindi cha jua.

**Maximum temperature** Kiwango cha juu zaidi cha halijoto katika anga hewa katika kipindi maalumu.

**Mean temperature** Hali ya joto wastani ; hali joto ambayo huafikiwa kutokana hesabu ya vipimo vingi vya hali ya joto vilivyorekodiwa katika kipindi maalumu kama vile; siku au mwezi.

**Minimum temperature** Kiwango cha chini sana cha halijoto katika kipindi maaluumu.

**Mist** Mkusanyiko wa matone madogomadogo ya maji yanayounda kitu kama mawingu lakini huwa angani au karibu sana na ardhi na huzuia mtu kuona mbali lakini si kama ukungu.

**Moderate probability** Uwezekano wa kadri wa kutendeka kwa jambo Moderate rain Mvua wastani.

**Monsoon** Monsuni; pepo za msimu zitokazo Baharini na kuelekea nchi kavu.

## N

**Near average (normal)** Karibia wastani

# O

**Overcast** Utandu mawingu ; hali ya mawingu kutanda kote angani.

**Ozone** Ozoni; aina ya hewa, aina ya okisijeni iliyoko angahewa.

**Ozone layer** Utandu ozoni: utandu wa hewa ya ozoni ambao huzuia miale hatari ya jua kufika ardhini.

# P

**Partly cloudy** Mawingu machache. ; Hali ya hewa ambayo kati ya asilimia 30;70 huwa imetanda mawingu wakati wa usiku.

**Precipitation** Kunyesha; jina la kijumla liitwalo aina yoyote ya maji yanyeshayo kutoka mawinguni kama vile; mvua, manyunyu, mvua ya mawe na theluji. Hata hivyo, umande, ukungu na jalidi sio baadhi yake

**Pressure** Kanihewa ; shinikizo la hewa linaloisukuma hewa kwenye ardhi. Shinikizo hili la hewa huwa tofauti katika maeneo mbalimbali.

**Prevailling wind** Upepo wa kawaida; upande ambao upepo huvuma kutoka katika eneo fulani.

**Probabilistic forecast** Utabiri wa uwezekano wa kutokea jambo.

**Probability** Uwezekano.

# R

**Radar** Rada; chombo cha kielektroniki ambacho hu tumiwa na wanametrolojia kuangaza mvua au theluji au wanamaji na wanahewa kuangazia vitu vilivyokaribu na eneo lao.

**Radiation** Mvuke na vuguvugu unaotoka kutoka kwa kitu kwa mfano jua.

**Rain** 1. Kitendo cha kuanguka kwa matone ya maji kuto ka mawinguni
2. matone ya maji yanayoanguka kutoka mawiguni.

**Rain bow** Upinde wa mvua; upinde wenye umbo la uta na wenye rangi saba unaoonekana katika angahewa karibu na mawingu wakati ambapo miali ya jua inapita katikati ya mvua na kuchipuka.

**Rainfall** Kunyesha kwa Mvua;  matone ya maji ambayo hum wagika kutoka mawinguni.

**Rain gauge** Kipima mvua: kifaa kinachotumiwa kupima mvua inayonyesha.

**Rain shadow** Demani; sehemu ya kitu kama vile mlima ambayo huwa ambao upepo huelekea na aghalabu huwa umekauka kutokana na hali ambapo upepo huo hupoteza unyevunyevu ambao husababisha  mvua kabla ya kufika upande huo. M.f. mji wa Nanyuki uko demani mwa Mlima Kenya.

# S

**Scattered showers** Mvua kubwa ya muda mfupi inayonyesha pahali fulani na kukosekana kwengine; mvua ambayo hunyesha katika baadhi ya sehemu za eneo fulani huku nyingine zikikosa kunyesha

**Sea breeze** Upepo wa bahari/ matlai; upepo mwanana uvumao mchana kutoka baharini kwenda nchi kavu na huwa na hali joto ya chini

**Sea Level Rise** Kiwango cha upwaji wa bahari hususan kati ya kiwango wastani cha juu na chini zaidi.

**Sea surface temperatures** Hali ya joto ya baharini.

**Seasonal** Kitu ambacho huja kwa Majira / kipindi / msimu.

**Seasons** Majira/ misimu; vipindi tofautitofauti vya hali ya hewa na aghalabu hubadilikabadilika; husababishwa na hali ya nchi kubadilibadili mahali pake kadri jua linavyosonga;mfano majira ya baridi , vuli, joto, n.k.Vipindi hivi hutokea wakati tofautitofauti katika mwaka.

**Severe storms** Dhoruba kali.

**Severe weather** Hali mbaya ya hewa; hali yoyote ile ya hewa ambayo husababisha maangamizi kwa mfano, dhoruba, mvua ya mawe, mvua ya radi, na miale ya radi ambayo inatishia maisha ya viumbe k.v wanyama na binadamu.

**Showers** Mvua kubwa ya muda mfupi usiozidi dakika the lathini.

**Slush** Theluji inayoyeyuka; tope laini ambalo huwa mchanganyiko wa chembechembe za barafu au theluji iliyoyeyuka; maji na vumbi na aghalabu rangi yake huwa ni kijivu au kahawia.

| | |
|---|---|
| **Snow** | Theluji; maji yenye chembechembe nyeupe za barafu ambayo hunyesha kama mvua. |
| **Snow flake** | Chembe ya theluji; vipande vidogo vidogo vya barafu ambavyo huanguka kama theluji. |
| **Snow storm** | Dhoruba ya theluji; mporomoko mkubwa wa theluji usababishwao na dhoruba kali. |
| **Soil moisture** | Unyevunyevu wa mchanga; hali ya mchanga kuwa na umajimaji hasa baada ya mvua kunyesha. |
| **Spring tide** | Bamvua kubwa. hali ya kujaa kwa maji ya bahari ambayo huambatana na mwezi mchanga na mwezi mpevu. |
| **Stable air** | Hewa shwari: hewa ambayo ni baridi kuliko mazingira yake haiwezi kwenda angani na haisababishi mawingu kwenda juu na haitengenezi mvua huwa wakati wa shwari |
| **Storm cloud** | Wingu dhoruba; aina ya wingu zito sana ambalo huwa ni ishara ya dhoruba. |
| **Storms** | Dhoruba; hali ya mchafuko wa angahewa unaosababisha mabadiliko ya hali ya hewa na aghalabu unaweza kuhusishwa na radi, miale ya radi na mvua kubwa. |
| **Stratus** | Mawingu nga'mba; aina ya mawingu bapa yenye rangi ya kijivu ambayo huwa karibu na ardhi kuliko mengine yote. |
| **Summer** | Majira ya joto; majira ya mwaka ya vuguvugu ambayo huanza mwezi wa sita na kukamilika mwezi wa tisa. |

**Sun** Jua; nyota kubwa Zaidi ya zote ambayo huchomoza mashariki na kutua magharibi na aghalabu hutoa miale ya mwangaza mchana.

**Sunny intervals** Kipindi cha mawingu na jua. ; Hali ambapo anga hutanda mawingu huku kukiwa na vipindi vifupi vya jua.

**Sunrise** Macheo; wakati ambapo jua huchomoza.

**Sunset** Machweo/mawio; wakati ambapo jua hutua.

# T

**Temperature** Hali joto; hali ya kuwa na joto au baridi joto ya mwili au angahewa ambayo hupimwa kwa kutumia kipima joto.

**Thermometer** Kipima joto; kifaa cha kisayansi cha kupimia kiasi cha joto katika angahewa au mwilini.

**Thunder** Radi; sauti ya mgurumo wa radi.

**Thunderstorm** Mvua ya radi aina ya mvua ya radi ambayo hushuhudiwa katika msimu wa joto na aghalabu huhusishwa na hewa vuguvugu yenye unyevunyevu; huanza kunyesha kutoka mchana hadi machweo.

**Tidal movements** Maji makimbizi.

**Tidal wave** Kabobo; mawimbi makubwa ya baharini yanayo haribifu vitu aghalabu hali hii hutokana na vo likano au mtetemeko wa ardhi wa majini. Huwa haina uhusiano wowote na kupwa au kujaa kwa maji baharini.

**Tide** Hali ya Maji kujaa na kupwa; hali ambapo maji husonga kutoka baharini kuelekea nchi kavu (ukingoni) mara kwa mara.

**Tide range** Tofauti kati ya maji kupwa na maji kujaa katka bahari

**Tornado** Kimbunga; upepo mkali ambao huvuma kwa nguvu sana na kuharibu vitu kama vile paa za mijengo na kuangusha miti.

**Tremor** Mtetemeko wa kiwango cha chini wa ardhi.

**Tsunami** Sunami; neno la kijapani lenye maana ya mawimbi makubwa baharini yasiyo ya kawaida na aghalabu husababishwa na mtetemeko wa ardhi.

**Typhoon** Tufani/ kimbunga; upepo mkali ambao huzunguka huku ukibeba vitu na vumbi hasa sehemu zilizoko Magharibi mwa Bahari Pasifiki

# U

**Unstable air** Hewa songezi; hewa ambayo ina joto jingi kuliko mazingira yake na hupanda juu angani na kutengeneza mawingu ya mvua.

# V

**Veering wind** Upepo unaobadili welekeo; upepo ambao hufululiza huku ukibadili welekeo wake

**Very heavy rainfall** Mvua kubwa sana; mvua inayonyesha kwa wingi na kwa kipindi kirefu na aghalabu huwa kati ya milimita 124.5; 244.5

**Very high wind** Upepo mkali sana;hewa ambayo huenda kwa kasi sana.

**Visibility** Hali ya uwezo wa kuona mbali kulingana na hali ya hewa.

# W

| | |
|---|---|
| **Warning** | Tahadhari. |
| **Watch** | Tahadhari; utabiri wa hali ya hewa ambao hutolewa na Shirika la Hali ya hewa la Kitaifa baada ya hatari ya hali ya hewa iliyokuwepo kuisha hivyo watu wanaweza kuendelea na shughuli zao za kawaida. |
| **Water vapour** | Mvuke; aina ya gesi iliyoko kwenye anga hewa ambayo huwa ni kati ya asilimia 1; 4 ya anga hewa; na aghalabu huchangia katika kutengeneza mawingu ya mvua na theluji. |
| **Weather** | Hali ya hewa; hali tofautitofauti ambazo husababisha mabadiliko kwenye anga hewa kama vile: upepo, mvua, hali joto, kipindi cha mawingu, hali tulivu n.k. na aghalabu hutokea katika kipindi maalumu katika eneo Fulani. |
| **Weather Advisory** | Ushauri wa hali ya hewa. |
| **Weather forecast** | Utabiri wa hali ya hewa; maelezo yanayotolewa kuhusu hali ya hewa pamoja na mabadiliko yanayotarajiwa wakati Fulani kama vile usiku, asubuhi n.k. ili watu wajiandae. |
| **Weather watch** | Tahadhari ya hali ya hewa. |
| **Wind** | Upepo; hewa ambayo huenda kwa kasi huku ikivuma |
| **Winter** | Kipupwe: Msimu wa ya baridi kali. |
| **World Meteorological Organisation** | Shirika la Hali ya hewa Duniani |

The Adaptation (ADA) consortium is a core component of the National Drought Management Authority strategy and funded within the Strengthening Resilience and Adaptation to Climate Change in Kenya plus (STARCK+) programme. The aim of the Adaptation Consortium is to pilot climate change adaptation planning approaches to enhance climate resilience in five Arid and Semi-Arid Lands (ASALs) counties (Garissa, Isiolo, Kitui, Makueni and Wajir) that, if successful, will be replicated in other ASAL counties and beyond. The consortium consist of Christian Aid working with ADS-Eastern in Kitui and Makueni, International Institute of Environment and Development (IIED) working with Resource Advocacy Programme (RAP) in Isiolo, WomanKind Kenya in Garissa,and Arid Lands Development Focus (ALDEF) in Wajiir, Met Office (UK) and the Kenya Meteorological Department (KMD).

The Kamusi was translated by GallaBABU Media creativity at its best

This research was funded by UK aid from the UK Government,however the views expressed do not necessarily reflect the views of the UK Government.

UKaid from the British people

©NDMA 2015

All rights reserved. No part of this publication may be reproduced, stored in a retrieval system, or transmitted, in any form or by any means, without the prior permission in writing from NDMA